Toleo la 17

# Jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Machi 14, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## MHE MAJALIWA: MICHEZO ITAENDELEA KUPEWA KIPAUMBELE NCHINI

WAZIRI MKUU. Mhe, Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa, Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kufanya jitihada mbalimbali kuhakikisha Sekta ya Michezo nchini inapiga hatua kwenda mbele kwakuwa michezo ni zaidi ya burudani.

Mhe. Majaliwa ametoa kauli hiyo, Februari 27, 2022 alipozungumza na wananchi wakati wa maadhimisho ya miaka 20 ya mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 katika Uwanja wa Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MOCU) mkoani Kilimanjaro. Mbio hizi zimeshirikisha wakimbiaji zaidi ya 12,000 kutoka mataifa zaidi ya 55 duniani huku wanariadha wa hapa nchini Tanzania ikiongoza katika mbio hizo.

Mhe. Waziri Mkuu amesema mbali na kuimarisha hali ya uchumi, michezo pia inaimarisha afya bora kwa kushiriki katika mazoezi au shughuli za nguvu kwa ajili ya kujikinga na maradhi ambayo yamekuwa yakiongeza gharama za matibabu na kupotea kwa nguvu kazi ya taifa.

Waziri Mkuu ametumia fursa ya mashindano hayo kutoa maagizo mujarabu kadhaa kwa Wizara mbalimbali kuhakikisha sekta ya michezo nchini inaendelea kuimarishwa kulingana na mahitaji na soko la sasa katika michezo duaniani.

Kwa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo pamoja pamoja na na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mhe. Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa ameziagiza wizara hizi kushirikiana na waandaaji wa mashindano ya Kilimanjaro Marathon ambao ni kampuni ya Executive Solutions kuona namna bora ya kutumia mbio hizo kutangaza zaidi fursa za utalii na vivutio mbalimbali vilivyopo hapa nchini kwa manufaa ya Taifa.

Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeagizwa kupitia mitaala ya Elimu Msingi kwa ajili ya kufundisha elimu ya michezo na kuanzisha vituo vya michezo (Sports Academy) ili watoto wenye vipawa waweze kulelewa na kukuza vipawa vyao.

Sisi Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, tunaipongeza Serikali kwa maamuzi na maelekezo haya maridhawa ya kuendeleza michezo nchini. Tunaamini Serikali inadhamira ya dhati ya kuinua na kuendeleza michezo hapa nchini, huu ni muda muafaka, kila mdau anapaswa kuwajibika kwa sehemu yake ili kuendelea kuimarisha sekta hii.

Ndiyo maana tunasema michezo ni afya, udugu na ni uchumi, hivyo kazi iendelee kwa kila mtu ashiriki michezo kuunga mkono juhudi za Serikali kutokomeza magojwa yasiyoambukizwa ambayo dawa yake kuu ni michezo.

**Mhariri**
John Mapepele

## BODI YA WAHARIRI

**Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**
Dkt. Hassan Abbasi

**Mhariri**
John Mapepele

**Waandishi**
Adeladius Makwega
Shamimu Nyaki

**Wapiga Picha**
Joseph Kigingi
Projestus Binamungu

**Kona ya Kiswahili**
Eleuteri Mangi



# Timu ya Wanawake U17 kuitwa Serengeti Girls- Mhe. Mchengerwa

Na. John Mapepele

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa amewakata wachezaji wa timu ya soka ya wanawake chini ya umri wa miaka 17 kucheza kombe la dunia litakalofanyika nchini India mwaka huu, huku akiipa jina la Serengeti Girls na kutaka waendeleze kipigo kwa mchezo wa marudiano wa kufuzu kombe la dunia dhidi ya Botwana utakaofanyika machi 20, 2022 nchini Botswana.

Mhe. Mchengerwa ametoa kauli hiyo Machi 11, 2022 baada ya kuitembelea timu hiyo iliyo kaa kambini Zanzibar tangu Februari 23, 2022 ambako inaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wa marudiano na timu ya Botswana baada ya kuichabanga timu hiyo mabao saba kwa nunge.

Ameongeza kuwa watanzania wana matarajio makubwa na timu hiyo kuwa italinda na kutetea heshima Taifa letu ndiyo maana ameamua kuipa jina la Serengeti kwa kuwa hifadhi hiyo ina heshima kubwa duniani kubwa.

“Nimeamua kuwapa jina hilo la Mbuga yetu ya Serengeti kutokana na ukweli kuwa Mbuga yetu inaheshimika ni matarajio yetu kuwa mtaendelea kutuheshimisha hata katika mchezo unaokuja hivi karibuni na wapinzani wetu Botswana”.amesisitiza Mhe. Mchengerwa




# Kiswahili Chapenya Umoja Wa Afrika

Na Mwandishi wetu - VPO

Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali umeridhia na kupitisha ombi la Tanzania la kutaka Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika Umoja huo.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango amewasilisha ombi hilo la lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha za kazi katika mikutano ya Umoja wa Afrika.

Dkt. Mpango ameongeza kuwa Kiswahili ni miongoni mwa lugha za kiafrika zenye wazungumzaji wengi barani hapo ambapo takribani watu milioni mia moja wanakitumia Kiswahili pamoja na wazungumzaji kutoka nje ya Bara la Afrika.

Kutokana na umuhimu wa lugha hiyo Makamu wa Rais amesema tayari inatumika katika jumuiya mbalimbali ikiwemo jumuiya ya Afrika Mashariki,Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na kufundishwa kwa lugha hiyo katika nchi nyingi za Afrika shuleni.

Amesema tayari Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni limetangaza tarehe saba Julai ya kila mwaka kuwa siku ya maadhimisho ya lugha Kiswahili Duniani.

Katika kupambana na Uviko19, Umoja wa Afrika umetoa rai kwa nchi kushirikiana katika kukabiliana na janga hilo ikiwemo kuhakikisha chanjo zinapatikana pamoja na kuyaunga mkono mataifa yalioanza jitihada za kuzalisha chanjo hiyo barani Afrika ikiwemo Afrika Kusini, Senagal na Rwanda.




# Mhe. Mchengerwa- Tanzania na China Kufufua uhusiano kwenye Utamaduni, Sanaa na Michezo

NNa. Adeladius Makwega

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema Serikali ya Tanzania inakwenda kufufua mpango wa miaka mitatu wa maendeleo ya Sekta za utamaduni, Sanaa na michezo na Serikali ya China.

Akizungumza Februari 4, 2022 jijini Dar es Salaam na Balozi wa China nchini Mhe. Chen Mingjian katika kikao maalum wakati wa sherehe za uzinduzi wa michezo ya msimu wa baridi ya Olympic 2022 amesema tayari wizara imeandaa andiko kwa ajili ya mpango huo litakalowasilishwa hivi karibuni.

"Tunatarajia kuwasilisha mpango wetu ambao tutaingia makubaliano ili utekelezaji wake uanze mara moja" amefafanua Mhe. Mchengerwa

Kwa upande wake Balozi Chen amesema ni wakati muafaka wa kufufua na kuendeleza sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kuinua uchumi wa nchi zote baada ya kushuka kutokana na ugonjwa wa Uviko 19.

Amesema Serikali yake itaendelea kuisaidia Tanzania katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu kupitia mafunzo mbalimbali.

"Awali watu wetu walikuwa wanapata fursa ya kuja Tanzania na watanzania kwenda China lakini kutokana uviko tulishindwa sasa ugonjwa umepita, Tunajipanga tuinue sekta zetu kwa pamoja" ameongeza Mhe. Balozi Chen

Amempongeza Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan kwa msimamo wake wa kuendelea kuenzi na kuendeleza uhusiano mzuri uliojengwa na viongozi waasisi wa mataifa hayo mawili ya muda mrefu.

Katika kikao hicho Mhe. Waziri aliambatana na Katibu Mkuu wa wizara Dkt. Hassan Abbasi



# Mhe. Mchengerwa Atoa Maagizo Mazito TaSUBa

**Na. John Mapepele**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe, Mohamed Mchengerwa ameitaka Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na wadau mbalimbali wakiwemo wazalishaji wa muziki hapa nchini kutengeneza muziki wa kitanzania ambao utalitambulisha taifa la Tanzania duniani.

Mhe. Mchengerwa amesema hayo Februari 9, 2022 alipofanya ziara ya kikazi kwenye taasisi hiyo mjini Bagamoyo akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wake Dkt. Hassan Abbasi na Naibu Katibu Mkuu. Saidi Yakubu.

Amesema kutokana na ukongwe wa chuo hicho ni muhimu kikafanya kitu kikubwa ambacho kitasaidia kuutambulisha utamaduni wa Tanzania duniani na kutoa ajira kwa vijana wengi.

Aidha Mhe, Mchengerwa ameitaka Wizara yake kuanzisha kituo cha Televisheni na Redio kitakachokuwa na studio maalum ambayo itasaidia kuzalisha, kukuza na kunoa wasanii kutoka mitaani na vijijini nchi nzima, pia viongozi wa sanaa na wafanyakazi katika sekta ya utamaduni sambamba na kuzalisha kazi za sanaa pamoja na huduma za medianuai (multimedia).

Mkakati wa kusaka vibaji vya wasanii mtaa kwa mtaa nchi nzima ni jambo alililoliasisi Mhe. Mchengerwa mara baada ya kuteuliwa hivi karibuni kuiongoza Wizara hiyo ambapo sasa anataka kuanzishwa kwa kituo cha televisheni na redio ambacho kazi yake kitakuwa kikitangaza maudhui ya Utamaduni na Sanaa za kitanzania pia michezo mbalimbali ili kuuza utamaduni wa mtanzania kimataifa.

Aidha, Mhe. Mchengerwa ameelekeza TaSUBa kuanza mara moja maandalizi ya Tamasha la kimataifa la Sanaa na Utamaduni la mwaka huu ili liwe bora zaidi kuliko matamasha yote yaliyotangulia pia kutangaza utamaduni kama bidhaa ya utalii kimataifa.

"Naelekeza sasa tujipange kuanzia sasa kwa ajili kuandaa tamasha hili la kimataifa la utamaduni na sanaa na tushirikiane na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya nje kulitangaza nje ya mipaka ya nchi yetu na tuwakaribishe wageni." Amesisitiza Mhe. Waziri




# Mhe. Mchengerwa Aagiza Bakita Kuratibu Siku Ya Kiswahili Duniani Kimkakati

**Na. John Mapepele**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe, Mohamed Mchengerwa ameliagiza Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kuratibu Siku ya Kiswahili Duniani kwa kushiriana na Wizara ya Mambo ya Nje na wadau mbalimbali ikiwa ni mkakati wa makusudi wa kuibidhaisha lugha hiyo duniani

Kauli hiyo ameitoa Februari 9, 2022 jijini Dar es Salaam kwenye Ofisi za BAKITA alipotembelea, kukagua shughuli za BAKITA kwa mara ya kwanza baada ya kuteuliwa kuwa Waziri mwenye dhamana Utamaduni, Sanaa na michezo ambapo pia ameambatana na Katibu Mkuu wa Wizara yake Dkt. Hassan Abbasi.

Amesema kwa vile siku hii imetambuliwa duniani na imeshatangaza kuwa lugha ya kazi kwenye Umoja wa Afrika ni lazima kuipa umuhimu wa kipekee na kuiandaa kwa kuitangaza kwa nguvu zote ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kimkakati ambapo ametaka kila ubalozi wa Tanzania duniani kuadhimisha siku hii kikamilifu.

Akifafanua amesema maandalizi hayo yanatakiwa kuhusisha wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine wanamchango katika kukuza na kubidhaisha lugha ya Kiswahili na amesisitiza kuanza mapema ili kutoa nafasi ya watu wengi kupata ujumbe ambao unatakiwa kutolewa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyommbo vya habari.

"Ninataka mtoke mwende mkabidhaishe kiswahili, pia andaeni kanzidata inayoainisha wataalam tulionao, kiwango chao cha elimu ili tuone wakihitajika tunawapata wapi" amesisitiza Mchengerwa.

Amepongeza juhudi zilizofanywa na Muasisi wa taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere za kuingiza lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa kupitia Chama cha Siasa cha TANU mwaka 1954 na Rais wa awamu ya Tano hayati John Pombe Magufuli kwa kukipigania Kiswahili ili kiwe lugha ya kimataifa na sasa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa msitari wa mbele kukibidhaisha Kiswahili duniani.

Pia amesema BAKITA linahitaji kuboresha miundombinu ya mitandano kwa ajili ya kazi mbalimbali za kukuza, kueneza na kuhifadhi Kiswahili.

Akiwa ofisini hapo alipata fursa ya kutembelea darasa lenye mitambo ya kisasa zaidi barani Afrika kwa ajili ya kufundishia ukalimani.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji wa Baraza hilo Consolata Mushi amemhakikishia Mhe. Waziri kuendelea kubidhaisha Kiswahili ambapo amesema katika siku za hivi karibuni wamekisajili kituo cha kufundisha Kiswahili nchini Ethiopia.







# Mhe. Mchengerwa Kufanya Dhukuru na Wadau wa Filamu

**Na. John Mapepele**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa Februari 12, 2022 ataanza kufanya dhukuru na wadau wa sekta ya Filamu jijini Dar es Salaam ikiwa ni mkakati wa makusudi wa kufanya tafakuri ya pamoja na wadau mbalimbali wa sekta anazoziongoza ili kutatua changamoto zinazowakabili na kuleta mapinduzi ya haraka.

Hayo yameelezwa Februari 11, 2022 jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dkt. Hassan Abbasi wakati akizindua rasmi Tamasha la Muziki la Serengeti litakalofanyika mwezi Machi Dodoma.

Amesema kundi la kwanza analokutana nalo kesho litahusisha wadau mbalimbali wa filamu ambao ni pamoja na watayarisha,waongozaji, wapiga picha, waandika miswada, waigizaji, wahariri na walimu kutoka shirikisho la filamu.

Akizungumza alipotembelea Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) hivi karibuni Mhe. Mchengerwa ameielekeza TaSUBa na wadau mbalimbali wakiwemo wazalishaji wa muziki hapa nchini kuandaa muziki wa kitanzania ambao utalitambulisha taifa la Tanzania duniani.

Aidha, katika hotuba yake ya kwanza kwenye hafla ya utoaji wa tuzo za muziki Mhe.Mchengerwa amesisitiza kuwa Wizara yake inakwenda kufungua milango kwa wadau mbalimbali wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kujadili kwa pamoja changamozo wanazokabiliana nazo na kuzimaliza katika kipindi kifupi."

"Sisi kama Wizara yenye dhamana ya utamaduni, Sanaa na michezo tunawaahidi wadau wetu kuwa karibu nao ili kuleta mapinduzi makubwa kwenye maeneo hayo hivyo nawaomba watumishi kufanya kazi kwa kasi na weledi wa hali ya juu, sitamvumilia mtumishi yoyote, mvivu na mzembe." amesisitiza Mhe. Mchengerwa.



# Mhe. Mchengerwa Dkt. Abbasi kushiriki kilele cha Tamasha la Sauti za Busara

**Na. John Mapepele**

Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa Februari 13, 2022 ameshiriki kwenye kilele cha Tamasha la kimataifa la Sauti za Busara la mwaka huu mjini Zanzibar.

Tamasha la Sauti za Busara ni miongoni mwa matamasha makubwa nchini ambayo yamefanikiwa kuonesha utamaduni wa nchi ya Tanzania duniani kupitia Sanaa za muziki.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi ambaye pia anashiriki amesema tamasha la mwaka huu limeboreshwa zaidi ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Dkt. Abbasi amesema kutokana na tamasha hilo amejifunza mengi ambayo yanaweza kusaidia kuboresha matamasha yanayokwenda kuandaliwa hivi karibuni.

"Tumejifunza mengi katika tamasha hili, kazi iliyombele yetu ni kubeba mambo mazuri ya tamasha hili kuboresha matamasha yanayokuja mbele yetu yawe kwenye hadhi ya kimataifa ili kuitangaza Tanzania na kuuza utamaduni wetu duniani, kama tulivyo elekezwa na Rais wetu kipenzi, Mhe. Samia Suluhu Hassan" ameongeza Dk. Abbasi

Awali Rais Samia katika tamasha la utamaduni la mkoa wa Kilimanjaro alielekeza Wizara ya utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana na wadau kuandaa matamasha makubwa ambayo yatasaidia kutangaza utalii na utamaduni wa Taifa la Tanzania kimataifa.

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar Mhe, Hussein Alli Mwinyi ameliezea Tamasha la Sauti za Busara kuwa lina mchango muhimu wa kuhamasisha umoja na mshikamano nchini.







# Serikali Imetenga Bilioni 19 Kwa Ajili Ya Shule Maalum 56 Za Michezo

**Na Shamimu Nyaki**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema Wizara katika bajeti ijayo imejipanga kujenga viwanja vya kisasa ambapo itaanza na mikoa 10 vitakavyoenda sambamba na mpango wa kuboresha miundombinu na vifaa vya michezo katika shule teule 56.

Mhe. Mchengerwa amesema hayo katika kikao kazi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Innocent Bashungwa na viongozi wa Wizara zenye dhamana ya Elimu, Michezo na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

"Kiu na ndoto ya Watanzania ni kushiriki na kufika kwenye ligi za kimataifa, kilio chao ni kutokuwa na miundombinu ya michezo vilevile kutowaandaa Watanzania kushiriki katika michezo mbalimbali wakiwa bado katika maeneo ya chini kwenye msingi, hivyo Serikali tumejipanga kuondoa kero hiyo ili sekta ya michezo ikue na itangaze nchi yetu"amesema Mhe. Mchengerwa

Kwa upande wake Waziri Bashungwa ameeleza kuwa uboreshaji wa miundombinu ya michezo na vifaa kwa ajili ya shule teule 56 za michezo utagharimu shilingi bilioni 19 na utaenda sambamba na kujenga shule za sekondari za kanda ambapo wanamichezo watakaopatikana katika shule hizo maalum wataweza kupatiwa nafasi ya kuendeleza vipaji na vipawa vyao katika shule hizo za kanda.

"Serikali imetenga Shule maalum 56 za Sekondari nchi nzima kwa ajili ya kukuza na kuendeleza vipaji mbalimbali vya michezo nchini vile vile kuanzisha shule za sekondari za kanda kwa ajili ya kuendeleza uboreshaji wa somo la elimu ya michezo nchini" amesisitiza Mhe. Bashungwa.

Aidha, Waziri Bashungwa ameeleza kuwa katika kikao hicho wamekubaliana na kupitisha mpango mkakati wa kusimamia utoaji wa elimu ya michezo katika shule za msingi na sekondari wa miaka mitano unaobainisha malengo, namna ya utekelezaji na matokeo ili utumike kama dira kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu.

Chimbuko la kuanzishwa shule za michezo lilitokana na kukosekana kwa utaratibu maalum wa kuendeleza vipaji kwa wanamichezo chipukizi waliopo shuleni, Tanzania kushindwa kufanya vizuri katika Mashindano ya kimataifa licha ya kuwa na vipaji vingi na kuzorota kwa ufundishaji wa somo la michezo katika shule za msingi na sekondari.



# Naibu Waziri Gekul: Wasanii zalisheni Kazi Bora Zinazokubalika Kimataifa

Na Eleuteri Mangi

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul amekutana na Wasanii wa tamthilia ya Huba na kufanya nao mazungumzo juu ya kuboresha kazi zao ili zikubalike ndani ya nchi na kimataifa.

Mazungumzo hayo yamefanyika Februari, 18, 2022 katika ofisi za wizara hiyo zilizopo Mtumba jijini Dodoma ambapo wasanii hao walipata fursa pia kutembelea ujenzi wa jengo jipya la wizara hiyo.

"Asanteni kwa ziara yenu ya kutembelea ofisi zetu hapa Mtumba mji wa Serikali, kwetu sisi ni heshima na faraja. Huo ni uungwana na upendo, sisi tunauthamini jitihada zenu. Hakika tamthilia yenu ya Huba ni nzuri, watu wanaifuatilia sana" amesema Mhe. Gekul.

Akiongea na wasanii hao, Naibu Waziri Gekul amesema kuwa wizara hiyo imekuwa sikivu na inaendelea kusimamia sekta zilizo chini yake kwa kuzingatia maelekezo ya Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan ambayo kila mara amekuwa akisistiza Serikali inapaswa kuwa karibu na wadau wake.

Kwa upande wake Rais wa Shirikisho la Filamu Tanzania Bw. Eliya Mjatta amesema tamthilia Huba imekuwa jukwaa la kuitangaza nchi Tanzania Zaidi ya miaka sita kimataifa kupitia kisimbuzi DSTV chaneli ya Maisha Magic Bongo.




# Mhe. Gekul Awafunda Wasanii

**Na. John Mapepele**

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul amewataka wasanii kuendelea kuboresha kazi zao ili waweze kunufaika nazo zaidi.

Mhe Gekul amesema hayo Februari 22, 2022 kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam wakati alipokutana na wasanii kutoka Umoja wa Wasanii Wanawake Tanzania (UWAWATA) ambapo ameutaka umoja huo kuwa mfano wa kuzingatia maadili kwa wasanii wanawake hapa nchini.

Ameelekeza Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kushirikiana na umoja huo kutafuta masoko ya kazi hizo.
Aisha, Mhe. Gekul ameielekeza Idara ya Maendeleo ya Sanaa kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Idara hiyo za BASATA, TaSUBa na Bodi ya Filamu kuandaa mpango wa mafunzo maalum ili kuwajengea uwezo wasanii kwa gharama nafuu. Vilevile amewataka wanawake kuunda vikundi vidogo vidogo na kwenda Halmashauri ili kupata fedha zisizokuwa na riba zinazotolewa kwa ajili ya wanawake.

Naibu Waziri Gekul pia, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe, Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa na kutoa wito kwa wasanii kuchangamkia fedha hizo.

Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dkt. Kiagho Kilonzo ametoa wito kwa UWAWATA kusajili kikundi hicho au msanii mmoja mmoja ili waweze kutambulika na kunufaika na kazi zao.

Aidha, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Bakari Gaima amefafanua kuwa tayari Serikali imeshatengeneza mifumo ya kielektroniki ambayo wasanii wanaweza kujisajili wakiwa mahali popote duniani.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Hidaya Njaidi ameiomba Serikali kuendelea kuwatumia Wasanii wanawake katika kampeni mbalimbali za maendeleo.

Njaidi ameiomba Serikali kuandaa Tamasha la Wasanii Wanaweke ili kusaidia kukuza vipaji vya wasanii wachanga na amempongeza Mhe. Rais kwa kushiriki kutengeneza Filamu ya Royal Tour ambayo itaitangaza Tanzania duniani.

Mhe. Gekul ametumia nafasi hiyo kuwakaribisha wasanii wa UWAWATA kushiriki kwenye tamasha kubwa la kihistoria la Muziki wa Serengeti litakalifanyika Machi 12, 2022 jijini Dodoma.




# Mhe. Gekul Asisitiza Programu ya Jogging Mtaa kwa Mtaa

Na. John Mapepele

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe, Pauline Gekul amezitaka Halmashauri zote nchini kuhamasisha programu ya kufanya mazoezi kuanzia ngazi ya mtaa ili kuimarisha afya kwa jamii na kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan za kuibua vipaji vya michezo kuanzia ngazi ya chini.

Mhe. Gekul amesema hayo Februari 20, 2022, alipokua Mgeni Rasmi kwenye kilele cha Bonanza kubwa lililoandaliwa na Umoja wa Vilabu vya jogging klabu Mbagala, Mtoni Kijichi jijini Dar es Salaam mara baada ya kumaliza mbio za takribani kilomita 7.5 kuanzia Mbagala hadi Mtoni Kijichi.

Amezitaka Klabu za Mazoezi kote nchini kuhakikisha zinashirikisha kikamilifu makundi maalum ya jamii kwenye siku za mazoezi, huku akitoa pongeza kwa umoja wa Mbagala Jogging Klabu kwa kuandaa tamasha hilo ambalo amelielezea kuwa limekuwa la mafanikio makubwa.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi wote kutenga muda kila siku kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao.

"Akina mama wenzangu ujanja ni kufanya mazoezi ili kuboresha afya na mazoezi." Ameongeza Mhe. Gekul

Aidha, amezitaka Halmashauri zote nchini zikumbuke kutenga fedha kwa ajili ya michezo kwenye bajeti ya mwaka 2022/23 ili zisaidie shughuli za Michezo.
Katika hatua nyingine Mhe. Gekul ametoa rai kwa wanamuziki kuacha mara moja tabia ya kuingiza vionjo kwenye Wmbo wa Taifa kwani kwa kufanya hivyo wanaondoa uhalisia wa wimbo huo.

Tamasha hilo limebebwa na ujumbe "Michezo, Afya Uchumi na ndoa.




# Dkt. Abbasi azindua rasmi Serengeti Music Award 2022

Na. John Mapepele

Katibu Mkuu wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Dkt, Hassan Abbasi Februari 12, 2022 amezindua Tamasha la Muziki la Serengeti la mwaka huu jijini Dar ES Salaam.

Akizindua Tamasha hilo mbele ya Waandishi wa Habari, Dkt. Abbasi amesema tamasha la mwaka huu linakusudia kutangaza Utamaduni na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini.

Aidha amesema tamasha hilo litakuwa na zaidi ya wasanii 50 na litashirikisha wasanii wa lebo zote.

Ameongeza kuwa wasanii wakongwe na wachanga watashiriki ili kuleta radha tofauti tofauti.



# TaSUBa Yahimizwa kuwa ya Kimataifa

Na. John Mapepele

Naibu Katibu Mkuu wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Saidi Yakubu ameutaka uongozi wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) kuifanya taasisi hiyo kuwa kituo chenye hadhi ya kimataifa kwenye utoaji wa taaluma ya Sanaa na utamaduni kuliko ilivyo sasa.

Yakubu amesema hayo Februari 7, 2022 alipofanya ziara chuoni hapo na kuongea na watumishi na Menejimenti ya TaSUBa na baadaye kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi hiyo.

Amefafanua kuwa kutokana na upekee wa taaluma zinazotolewa na chuo hicho ambazo zinaendana na vyuo vya kimataifa hakuna sababu ya chuo hicho kubaki na hadhi yake ya sasa inayoongozwa na dira ya kutoa taaluma katika ubora kwa ngazi ya Afrika.

" Ni wazi kwamba kwa upekee wa chuo chetu na kozi zinazotolewa hapa ni lazima tuondokane na na fikra za Bagamoyo, Tanzania au hadhi ya Afrika na badala yake tuwe wa kimataifa " ameongeza Yakubu.

Ameutaka uongozi kuwa mbunifu kwa kutumia raslimali za wizara mama kujitanua zaidi nchi nzima badala ya kufikiria eneo la Bagamoyo pekee.

Amekitaka chuo kuongeza udahili wa wanachuo ili hadhi ya chuo hicho iwe ya kimataifa ambapo amesisitiza kuwachukua pia wanafunzi kutoka nje ya Tanzania ili wawe mabalozi wa kukitangaza chuo katika nchi zao.




# Yakubu: TTA Shirikianeni Na Serikali Kukuza Mchezo Wa Tenis

Adeladius Makwega

Serikali imevitaka vyama vya michezo nchini kushirikiana kwa karibu na serikali ili kufanikisha ukuaji wa michezo nchini.

Kauli hiyo imetolewa Februari 16, 2022 Mtumba jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu wa Utamaduni Sanaa na Michezo Saidi Othman Yakubu wakati akizungumza na Rais wa Chama Cha Mchezo wa Tenisi Tanzania ndugu Denis Makoi.

"Sisi tupo tayari na tunashirikiana vizuri na mashirikisho, vyama vyote vya michezo nchini, na tunawakaribisha sana kwa ajili ya kushirikikana ili ushindi wa timu zetu ya Tenisi upatikane ndani na katika mashindano ya kimataifa.

Ameongeza kuwa, Viongozi wa wizara hiyo wameweka utaratibu wa kuzungumza na wadau wote wa sekta na tayari wamekutana na BMT, huku akiahidi kukutana na wadau hao.

Ndugu Yakubu amepongeza chama hicho, kwa kutekeleza vizuri shabaha ya mchezo huo, kwani timu za mchezo huo tayari zimefuzu kushiriki katika mashindano kadhaa ya kimataifa.

"Jukumu letu sisi ni kuhakikisha timu zetu za taifa za michezo yote zilizofuzu zinashiriki mashindano yote ya kimataifa kwa gharama za serikali, jukumu la wachezaji wetu ni kucheza kwa bidii, moyo na uzalendo ili kuleta ushindi kwa taifa letu." amesisitiza Ndugu Yakubu

Awali Rais wa TTA nchini ndugu Makoi amesema kuwa anaishukuru serikali kwa kuwapa mwongozi mzuri wa kukiongoza chama cha mchezo huo ambao umetoa mwanga mpya kwa mchezo wa Tenisi nchini.

"Changamoto zetu zote nimeziwasilisha kwa serikali, ikiwemo la uhaba wa pesa na hilo serikali imetuhakikishia kulitatua kupitia bajeti ya wizara na wadau wengine wa michezo nchini." amesema Ndugu Makoi.



# Mhe. Mchengerwa Aipongeza Wasafi Kwa Kukuza Vipaji Vya Wasanii

**Na. John Mapepele**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa ameipongeza Kampuni ya Wasafi kwa kukuza sanaa ya muziki na kuzalisha ajira kwa vijana wengi hapa nchini.

Akizungumza kwenye hafla ya Usiku wa Mahaba Ndi Ndi Ndi siku ya wapendanao Februari 14, 2022 jijini Dar es Salaam amesema Wasafi ina mchango mkubwa katika kuibua na kukuza vipaji vya wanamuziki.

"Naomba nikuhakikishie Serikali ipo pamoja na nyie katika kukuza sanaa " amesema Mhe.Mchengerwa

Aidha, amesema Serikali inakwenda kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wasafi mtaa kwa mtaa, kijiji kwa kijiji hadi mkoa kwa mkoa kutafuta vipaji vya wasanii lengo ni kuwashindanisha na kuwaendeleza.

Ameongeza kuwa, wizara inakwenda kuendeleza mapinduzi ya ukuzaji wa Sanaa ili kutoa ajira zaidi kwa vijana katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Amefafanua kwamba kufanya hivyo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya kutaka kuboresha sekta hiyo ili wasanii nchini waweze kunufaika na kazi zao.

Kwa upande mwingine Mhe. Mchengerwa amesema, katika kipindi hiki sanaa inakwenda kutumika kuitangaza Tanzania kimataifa.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wasafi, Msanii nguli wa muziki wa kizazi kipya barani Afrika, Diamond Platinum ameishukuru Serikali kwa kuendelea kujenga mazingira wezeshi kwenye Sekta ya Sanaa nchini.

# Mhe. Dkt, Mpango Mgeni Rasmi Kongamano la Idhaa za Kiswahili duniani




Na. Eleuteri Mangi

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango anatarajiwa kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Kongamano la Pili la Idhaa za Kiswahili duniani ambalo litafanyika kwa siku tano kuanzia Machi 14-18, 2022 katika Ukumbi wa Kimataifa (AICC) jijini Arusha.

Hayo yamesemwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Bw, Saidi Yakubu wakati wa Mkutano na Waandishi wa Habari Machi 12, 2022 jijini Arusha ikiwa na maandalizi ya kuelekea ufunguzi wa kongamano hilo.

“Lengo la Kongamano hili ni kuwakutanisha pamoja Waandishi wa Habari na Watangazaji wa Idhaa zote duniani zinazotumia lugha ya Kiswahili ili kuangalia wanavyotumia lugha hii katika shughuli zao za kihabari, kubainisha changamoto wanazokutana nazo na jinsi ya kuzitatua” amesema Naibu Katibu Mkuu Bw. Yakubu.

Hadi sasa washiriki kutoka vyombo vya habari mbalimbali vya ndani na nje ya nchi wamethibitisha kushiriki kongamano hilo ambapo zipo redio za hapa nchini ni 45, redio za nje ni 15, televisheni za kawaida na za mtandaoni ni 13, Televisheni za nje ya nchi mbili, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya ndani 20, wachapishaji watano, watu mashuhiri kutoka ndani na nje ya nchi 16 pamoja na wanafunzi 200 kutoka vyuo vikuu vya jijini Arusha.

Washiriki hao wanajumuisha wawakilishi wa idhaa za Kiswahili za ndani na nje ya nchi, wataalamu wa Kiswahili na viongozi mbalimbali wa asasi za Kiswahili zinazoji-shughulisha na maendeleo na ufadhili wa shughuli za kukiendeleza Kiswahili.

Aidha, Kongamano ambalo litaangazia pia jitihada za vyombo vya habari katika ubidhaishaji wa lugha adhimu ya Kishwahili duniani na linatarajiwa kufungwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi Machi 18, 2022.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili la Taifa. Bi, Conso-lata Mushi amesema kuwa kongamano hilo litakwenda sanjari na uzinduzi wa Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la Tatu, uzinduzi wa mfumo wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa njia ya mtanadao, uzinduzi wa kitabu cha matumizi ya TEHAMA katika tasnia ya Habari pamoja na uwasilishwaji wa mada 10 za kitaaluma kutoka kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu na wataalamu mbalimbali wa lugha ya Kiswahili

Washiriki wa Kongamano hilo wanatoka katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Marekani, Rwanda, Ufaransa, Uganda, Ujerumani na wenyeji Tanzania.

Wazo la kuandaa Kongamano la Idhaa za Kiswahili Duniani lilianzishwa Novemba 29, 2006 na Kongamano la kwanza lilifanyika Novemba 12-15, 2007 ambapo lengo lake likiwa ni kuimarisha uhusiano na vyombo vya habari ambavyo vinatekeleza jukumu la kukieneza Kiswahili duniani kwa kukitumia na kutangaza katika vituo vyao vya habari.

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU

**Mawasiliano**
S.L.P 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@michezo.go.tz